



ISSN 0856-6976

---

# **MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA**

**2020/21**

---

**GAVANA  
BENKI KUU YA TANZANIA**

**Juni 2020**





ISSN 0856-6976

---

# **MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA**

## **2020/21**

---

**GAVANA  
BENKI KUU YA TANZANIA**

**Juni 2020**





## **Utangulizi**

Kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197, Kifungu cha 21(3) hadi (6) kinaitaka Benki Kuu kutoa Tamko la Sera ya Fedha mwanzoni mwa mwaka wa fedha, ikifuatiwa na tathmini ya nusu mwaka ambayo huonesha maendeleo katika utekelezaji wa sera ya fedha. Tamko hili linajumuisha mapitio ya mwenendo wa uchumi wa dunia na wa ndani na tathmini ya matokeo ya utekelezaji wa sera ya fedha ya mwaka 2019/20. Aidha, tamko linaonesha mwelekeo wa uchumi wa dunia na wa ndani na kuainisha malengo ya sera ya fedha kwa mwaka 2020/21 yanayoendana na mahitaji ya malengo mapana ya kiuchumi ya Serikali. Pamoja na hayo, tamko hili linaainisha hatua ambazo Benki Kuu itazichukua katika kutekeleza sera ya fedha kwa mwaka 2020/21 ili kufikia malengo hayo.

## **Mwenendo wa Uchumi wa Dunia**

Uchumi wa dunia ulikua kwa wastani wa asilimia 2.9 mwaka 2019, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.6 mwaka 2018, hii ikiwa ni kasi ndogo zaidi ya ukuaji tangu mdororo wa kiuchumi wa mwaka 2008. Hali hii ilichangiwa na kuongezeka kwa vikwazo vya kibishara baina ya China na Marekani, hali iliyopelekea kutokutabirika kwa mazingira ya biashara na shughuli za kiuchumi. Vilevile, mazingira magumu ya kifedha kwenye soko la dunia, mivutano ya kisiasa baina ya mataifa na machafuko katika baadhi ya nchi yalichangia kuongeza changamoto katika uchumi wa dunia.



Mwaka 2020, uchumi wa dunia unatarajiwa kuingia kwenye mdororo kutokana na athari za mlipuko wa ugonjwa unaosababishwa na virusi vya Corona (COVID-19), ambao umeathiri uchumi wa nchi mbalimbali kupitia kupotea kwa nguvu kazi na kuharibika kwa mnyororo wa ugavi kutokana na njia zilizotumika katika kudhibiti ueneaji wa ugonjwa huu. Kwa mujibu wa Taarifa ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*), ukuaji wa uchumi wa dunia unatarajiwa kupungua kwa asilimia 3.0 mwaka 2020, na hatimaye kuimarika hadi kufikia ukuaji wa asilimia 5.8 mwaka 2021. Uchumi wa mataifa yaliyoendelea unakadiriwa kupungua, wakati uchumi wa nchi zinazoibukia kiuchumi na zile zinazoendelea kukua ukitarajiwa kuwa na mwelekeo tofauti baina ya nchi moja na nyingine, japo kwa ujumla ukuaji wa uchumi wa nchi hizi unatarajiwa kupungua. Ukuaji wa uchumi wa nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara, unatarajiwa kupungua kwa asilimia 1.6 (ukuaji hasi) mwaka 2020 kabla ya kuongezeka hadi kufikia asilimia 4.1 mwaka 2021. Vilevile, makadirio ya ukuaji wa uchumi yaliyotolewa na mashirika mengine ya kiuchumi duniani, yanaonyesha mwelekeo wa ukuaji wa uchumi wa dunia unaofanana na wa mashirika makubwa ya kimataifa. Ripoti ya Shirika la Maendeleo ya Kiuchumi (OECD) ya Juni 2020 inakadiria uchumi wa dunia kupungua kwa asilimia 6.0 (ukuaji hasi) mwaka 2020, kabla ya kuongezeka hadi kufikia ukuaji wa asilimia 5.2 mwaka 2021. Aidha, ripoti ya Benki ya Dunia iliyotolewa Machi 2020 inabashiri ukuaji wa uchumi wa nchi Kusini mwa Jangwa la Sahara kupungua kati ya asilimia 2.1 na asilimia 3.0 kwa mwaka 2020.



Mfumuko wa bei katika nchi zilizoendelea ulibakia katika viwango vya chini kutokana na kushuka kwa mahitaji, wakati hali ya mfumuko wa bei katika nchi zinazoibukia na zile zinazoendelea kiuchumi ukiongezeka kutokana na kupanda kwa bei za vyakula. Mfumuko wa bei katika nchi zilizoendelea ulikuwa wastani wa asilimia 1.2 katika kipindi cha Julai 2019 hadi Aprili 2020, wakati wastani wa mfumuko wa bei katika nchi zinazoibukia na zile zinazoendelea kiuchumi ukiwa asilimia 4.5. Mfumuko wa bei katika nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC) umeendelea kubakia katika kiwango kilichokubaliwa cha chini ya asilimia 8.0, ikiwa ni wastani wa asilimia 4.2 katika kipindi cha Julai 2019 hadi Aprili 2020 ukilinganisha na asilimia 1.9 kwa kipindi kama hicho mwaka 2018/19, kutokana na ongezeko la bei za vyakula. Katika nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), wastani wa mfumuko wa bei uliongezeka na kufikia asilimia 39.3 kutoka asilimia 9.8 kutokana na baadhi ya nchi kuwa na kiwango kikubwa cha mfumuko wa bei.

Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) linakadiria viwango vya mfumuko wa bei katika nchi zilizoendelea kupungua na kufikia wastani wa asilimia 0.5 mwaka 2020, kutoka asilimia 1.6 mwaka 2019 kutokana na matarajio ya kupungua kwa bei za nishati. Wakati huohuo, mfumuko wa bei katika nchi zinazoibukia kiuchumi na zile zinazoendelea unatarajiwa kupungua kidogo hadi kufikia wastani wa asilimia 4.6 mwaka 2020, kutoka asilimia 4.9 mwaka 2019. Katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara mfumuko wa bei unatarajiwa kuongezeka hadi kufikia asilimia 9.3 mwaka 2020, kutoka asilimia 8.4 mwaka 2019 kutokana na matarajio ya kuongezeka kwa bei za vyakula katika baadhi ya nchi za bara la Afrika.



## **Mwenendo wa Uchumi wa Tanzania**

### **Tanzania Bara**

Uchumi wa Tanzania umeendelea kuimarika na kukua kwa kasi ya wastani wa asilimia 7.0 mwaka 2019<sup>1</sup>, sawa na ukuaji wa mwaka 2018. Shughuli za ujenzi zimeendelea kuwa na mchango mkubwa kwenye ukuaji wa Pato la Taifa kwa miaka mitatu mfululizo kutokana na uwekezaji unaoendelea kufanywa na Serikali katika kuboresha miundombinu, zikichangia wastani wa asilimia 27.6 ya Pato la Taifa mwaka 2019. Shughuli nyingine za kiuchumi zilizokuwa na mchango mkubwa kwenye ukuaji wa Pato la Taifa ni kilimo (asilimia 16.2), uchimbaji madini (asilimia 10.3), pamoja na shughuli za usafirishaji (asilimia 9.4). Aidha, shughuli za kiuchumi zilizokua kwa kasi ya juu zaidi ni pamoja na madini (asilimia 17.7), ujenzi (asilimia 14.8), sanaa na burudani (asilimia 11.2), usafirishaji na uhifadhi (asilimia 8.7), na huduma za kiutawala (asilimia 8.4). Shughuli za kilimo zimeendelea kushikilia sehemu kubwa ya Pato la Taifa kiasi cha asilimia 26.6, ikifuatiwa na ujenzi (asilimia 14.3), biashara (asilimia 8.8) na uzalishaji viwandani (asilimia 8.5). Vilevile, hali nzuri ya hewa, upatikanaji wa uhakika wa nishati ya umeme pamoja na sera madhubuti za fedha na kibajeti zimeendelea kuchochea zaidi ukuaji wa uchumi.

Katika mwaka 2020, uchumi unatarajiwa kuendelea kuwa imara japo kwa kasi ndogo ya ukuaji ikilinganishwa na kasi ya ukuaji ya mwaka 2019, kutokana na athari za janga la ugonjwa wa

---

<sup>1</sup> Kizio cha mwaka 2015





COVID-19. Shughuli zitakazoathirika zaidi na COVID-19 ni pamoja na utalii (hoteli na malazi), shughuli za kijamii kama michezo, elimu na uuzaji wa bidhaa za mbogamboga na maua nje ya nchi. Kutokana na hali hii, uchumi unakadiriwa kukua kwa asilimia 5.5 mwaka 2020, ukichangiwa zaidi na: uzalishaji katika sekta ya kilimo kutokana na uwepo wa hali nzuri ya hewa; shughuli za uchimbaji wa madini kutokana na ongezeko la bei katika soko la dunia na usimamizi madhubuti wa sekta ya madini; uwekezaji wa serikali katika miundombinu; na sera nzuri za fedha na kibajeti. Matarajio haya ya ukuaji wa uchumi pia yanatokana na uamuzi wa Serikali wa kutofunga shughuli za kiuchumi kufuatia mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 (isipokuwa kwa shule na shughuli za kimichezo) mnamo Machi hadi Mei 2020; athari ndogo za janga la COVID-19 kwenye uchumi jumla zimetokana na kuwa na uchumi unaotegemea sekta zaidi ya moja, pamoja na matarajio ya kufunguliwa mapema kwa uchumi wa washirika wa kibiashara kuliko ilivyotarajiwa awali.

Mfumuko wa bei umeendelea kubakia ndani ya lengo la muda wa kati la asilimia 5.0 katika kipindi chote cha Julai 2019 hadi Aprili 2020, na ndani ya vigezo vya mtangamano wa kiuchumi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) usiozidi asilimia 8.0, na wigo uliokubalika katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) wa kati ya asilimia 3.0 na 7.0. Mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 3.6 katika kipindi cha Julai 2019 hadi Aprili 2020, ukilinganisha na wastani wa asilimia 3.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2018/19. Kasi ndogo ya mfumuko wa bei ilichangiwa zaidi na upatikanaji wa chakula cha kutosha, sera madhubuti za fedha na kibajeti, bei ndogo



ya mafuta na upatikanaji wa uhakika wa nishati ya umeme. Aidha, mfumuko wa bei usiojumuisha bei za vyakula na nishati ulikuwa wastani wa asilimia 2.4 ukilinganishwa na asilimia 2.7. Mfumuko wa bei unatarajiwa kubakia ndani ya lengo la muda wa kati la asilimia 5.0 katika mwaka 2020/21, kutokana na matarajio ya upatikanaji wa chakula cha kutosha, kupungua kwa mahitaji ya walaji, upatikanaji wa uhakika wa nishati ya umeme, bei ndogo za mafuta duniani na utekelezaji thabiti wa sera ya fedha na ya kibajeti.

Katika kipindi cha mwaka 2019/20, kiwango cha ukwasi katika uchumi kimeendelea kubaki katika viwango vinavyotosheleza mahitaji halisi ya shughuli mbalimbali za kiuchumi sambamba na malengo ya utekelezaji wa sera ya fedha. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa wastani wa asilimia 9.9 kwa kipindi cha Julai 2019 hadi April 2020, ikilinganishwa na lengo la ukuaji wa asilimia 10.0 na wastani wa asilimia 4.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2018/19. Vilevile, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) ulikua kwa wastani wa asilimia 11.4 ikilinganishwa na wastani wa ukuaji wa asilimia 5.2 kipindi kama hicho mwaka 2018/19, wakati wastani wa ukuaji wa fedha taslim ukiwa asilimia 7.0 ikilinganishwa na kuporomoka kwa ukuaji kwa asilimia 0.4 mwaka 2018/19. Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Aprili 2020, mikopo kwa sekta binafsi imeendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha ya wastani wa asilimia 8.7, ikilinganishwa na asilimia 6.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2018/19. Sehemu kubwa ya mikopo kwa sekta binafsi ilielekezwa kwenye shughuli binafsi za kiuchumi, biashara, viwanda na kilimo. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi kwa mwaka 2020/21 unatarajiwa kuendelea kuwa



imara, ukikadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 11.6. Makadirio haya yanazingatia utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi na hatua za kisera zilizochukuliwa na Serikali kwa ajili ya kupambana na athari za COVID-19 kwenye sekta ya fedha na uchumi kwa ujumla. Vilevile, kufunguliwa mapema kwa shughuli za kiuchumi zilizoathiriwa na janga la COVID-19 kama vile kuanza kwa shughuli za utalii, michezo, burudani na elimu kutachochea zaidi ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi.

Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Aprili 2020, utekelezaji wa bajeti ya serikali umebakia ndani ya malengo, licha ya kukabiliwa na changamoto kadhaa zilizosababishwa na COVID-19. Mapato ya ndani yaliyokusanywa na kuwekwa kwenye akaunti za Serikali zilizoko Benki Kuu ya Tanzania yalifikia shilingi bilioni 16,238.0, sawa na asilimia 95.5 ya makadirio ya makusanyo kwa kipindi hicho, ikiwa ni asilimia 10.5 zaidi ya makusanyo ya kipindi kama hicho mwaka 2018/19. Mwenendo huu wa ukusanyaji wa mapato umetokana na kuimarika kwa usimamizi wa ukusanyaji wa mapato uliotekelezwa na Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA). Jumla ya matumizi ya Serikali katika kipindi hicho yaliyopitia Benki Kuu ilikuwa shilingi bilioni 18,281.1, kati ya hizo matumizi ya maendeleo yalikuwa shilingi bilioni 5,284.9. Katika kukabiliana na changamoto za kiuchumi kutokana na ugonjwa wa COVID-19, Serikali, pamoja na mambo mengine, iliongeza matumizi katika sekta ya afya na huduma za jamii, kuondoa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na ushuru wa forodha kwenye vifaa tiba, na kulipa malimbikizo ya madeni kwa sekta binafsi. Deni la Serikali la ndani na nje limeendelea kubaki



katika viwango himilivu na kufikia dola za Marekani milioni 24,179.5 mwezi Aprili 2020, kutoka dola za Marekani milioni 23,215.4 mwezi Juni 2019. Kati ya kiasi hicho deni la nje lilikuwa sawa na asilimia 73.2.

Urari wa malipo nje ya nchi ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 897.1 katika kipindi cha Julai 2019 hadi Aprili 2020, ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,082.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2018/19. Hali hii ilichangiwa na kupungua kwa nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje. Nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje ilipungua kufuatia kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa nje ya nchi, hususan dhahabu na korosho.

Akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kuridhisha kukidhi mahitaji ya fedha za kigeni kwa ajili ya kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili 2020, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Marekani milioni 5,334.3, kutoka kiasi cha dola za Marekani milioni 4,432.6 mwezi Juni 2019. Akiba hiyo inatosha kulipia uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi 6.1, kiwango ambacho ni juu ya lengo la nchi la kukidhi miezi isiyopungua minne. Kwa mwaka 2020/21, mapato ya mauzo ya nje ya nchi yatokanayo na shughuli za utalii yanatarajiwa kupungua kutokana na athari za COVID-19. Aidha, wastani wa bei ya mafuta katika soko la duniani inakadiriwa kubaki katika viwango vya chini, wakati bei ya dhahabu ikikadiriwa kuongezeka na kubakia katika viwango vya juu.



Sekta ya kibenki kwa ujumla imeendelea kuwa imara na salama. Benki zimeendelea kuwa na viwango vya mitaji ya kutosha kuhimili misukosuko. Uwiano wa mtaji wa msingi wa sekta ya benki ukilinganishwa na jumla ya rasilimali ilikuwa asilimia 17.4 mwezi Aprili 2020, ikilinganishwa na kiwango cha chini cha kisheria cha asilimia 10.0. Aidha, uwiano wa ukwasi wa sekta ya benki kiujumla umeendelea kubakia kwenye kiwango cha juu cha asilimia 32.7, ikilinganishwa na kiwango cha chini cha kisheria cha asilimia 20.0. Wakati huo huo, uwiano wa mikopo chechefu kwenye mikopo yote uliongezeka na kufikia asilimia 11.0 mwezi Aprili 2020 kutoka asilimia 10.7 mwezi Juni 2019. Hatua za sera ya fedha na ya kibajeti zilizotekelezwa katika kupunguza athari za ugonjwa wa COVID-19 katika uchumi, kama vile kutoa unafuu wa mahitaji ya kiusimamizi katika kufanya marekebisho ya marejesho ya mikopo (*loan restructuring*), zinatarajiwa kupunguza kiwango cha mikopo chechefu. Vilevile, Benki Kuu inaendelea kuzitaka benki zote kutekeleza mipango madhubuti na mikakati ya kupunguza mikopo chechefu, na kuhimiza benki na taasisi za fedha kutumia kanzidata ya taarifa ya historia za wakopaji kabla ya kutoa mikopo mipya, ili kupunguza uwiano wa mikopo chechefu iweze kuzingatia kiwango kinachokubalika na Benki kisichozidi asilimia 5.0. Hatua nyingine ni pamoja na kutekeleza mfumo wa kumlinda mlaji (*consumer protection framework*) na kuwataka watumishi wa benki zote kufuata maadili ya kiutendaji yaliyoainishwa na Chama cha Mabenki Tanzania (*Tanzania Bankers Association Code of Conduct*).



Katika kipindi cha Julai 2019 mpaka Aprili 2020, mifumo ya malipo imeendelea kufanya kazi kwa ufanisi, ikiakisi ongezeko la matumizi ya kidigitali katika utoaji wa huduma za kifedha. Ongezeko la matumizi ya mifumo ya kidigitali katika utoaji wa huduma za kifedha kwa taasisi za umma na binafsi umepunguza gharama za uendeshaji pamoja na kuchangia katika shughuli za kiuchumi, kama vile ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Utoaji wa huduma za kifedha za kidigitali kupitia simu za mikononi umeendelea kuongezeka kwa kasi katika kipindi cha Julai 2019 hadi Aprili 2020. Katika kipindi hicho, miamala inayotumia simu za mikononi iliongezeka na kufikia milioni 177.0 ikiwa na thamani ya shilingi bilioni 5,209.9 sawa na ongezeko la asilimia 20.8 ikilinganishwa na miamala iliyofanyika katika kipindi kama hicho mwaka 2018/19; na ongezeko la asilimia 6.6 ikilinganishwa na thamani iliyopatikana katika kipindi kama hicho mwaka 2018/19. Hadi kufikia mwezi April 2020, Watanzania wapatao milioni 26.0 walikuwa watumiaji wa miamala kwenye mfumo wa malipo kupitia simu za mikononi, ikilinganishwa na Watanzania milioni 22.3 waliokuwepo mwishoni mwa mwezi Juni 2019. Katika kuhamasisha na kuongeza matumizi ya huduma za kifedha za kidigitali katika kufanya miamala mbalimbali, na hivyo kupunguza matumizi ya fedha taslim hususan katika kipindi cha janga la ugonjwa wa COVID-19, Benki Kuu kwa kushirikiana na watoaji wa huduma ya fedha kwa njia za kidigitali, wamekubaliana kuongeza ukomo wa miamala kwa siku kwa mteja kutoka shilingi milioni 3.0 hadi shilingi milioni 5.0, na kuongeza kiwango cha salio kwa siku kwa mteja kutoka shilingi milioni 5.0 hadi shilingi milioni 10.0. Aidha, Benki Kuu inaendelea kuhimiza mabanki kuongeza



matumizi ya mifumo ya kufanya miamala kwa njia ya kidigitali, ikiwemo matumizi ya mashine za kufanya malipo na kwa njia ya kielektroniki za kibenki.

## **Zanzibar**

Uchumi wa Zanzibar umeendelea kuwa imara ukikua kwa asilimia 7.0 mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 7.1 mwaka 2018. Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na huduma za hoteli, malazi na chakula, kufuatia kuongezeka kwa idadi ya watalii. Kwa mwaka 2020, ukuaji wa uchumi wa Zanzibar unakadiriwa kukua kwa asilimia 5.0, kufuatia athari za janga la COVID-19 katika shughuli mbalimbali za kiuchumi, hususan shughuli zinazohusiana na utalii, biashara na usafiri wa anga. Aidha, kama sehemu ya mkakati wa kuongeza vyanzo mbalimbali vya shughuli za kiuchumi ili kukuza Pato la Taifa, Serikali inawekeza kwenye shughuli za uvuvi na kilimo cha kibiashara.

Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Aprili 2020, mfumuko wa bei umeendelea kuwa tulivu katika viwango vya chini na kufikia wastani wa asilimia 3.6 kutoka asilimia 3.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2018/19. Mfumuko wa bei za vyakula uliongezeka hadi asilimia 4.9 kutoka asilimia 2.6, kutokana na kuongezeka kwa bei za bidhaa hususan unga wa mahindi, ndizi na sukari. Mfumuko wa bei usiohusisha bidhaa za vyakula ulipungua hadi asilimia 2.5 kutoka asilimia 4.0, kutokana na kushuka kwa bei ya mafuta. Aidha, mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kubakia katika viwango vya



tarakimu moja kwa mwaka 2020/21, licha ya changamoto za athari za janga la COVID-19 katika sekta mbalimbali za uchumi.

Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Aprili 2020, mapato ya ndani ya Serikali yalifikia shilingi bilioni 685.7, sawa na asilimia 82.4 ya makadirio ya makusanyo kwa kipindi hicho. Mapato ya kodi yalikuwa asilimia 80.6 ya lengo, wakati mapato yasiyo ya kodi yalikuwa asilimia 93.6 ya lengo. Kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato kumetokana na kuongezeka kwa jitihada na usimamizi wa ukusanyaji wa mapato uliofanywa na Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) pamoja na Bodi ya Mapato ya Zanzibar (ZRB). Aidha, kiwango cha mapato ya ndani kwa mwaka mzima wa 2019/20 kinakadiriwa kupungua ikilinganishwa na kiwango kilichopatikana mwaka 2018/19, kutokana na athari za janga la COVID-19 zilizosababisha mdororo kwenye shughuli za utalii na usafiri wa anga. Katika kipindi hicho, jumla ya matumizi ilikuwa shilingi bilioni 866.7, sawa na asilimia 94.1 ya makadirio, ambapo shilingi bilioni 611.7 zilikuwa za matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 255.0 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Katika kukabiliana na changamoto za kiuchumi kutokana na ugonjwa wa COVID-19, Serikali, pamoja na mambo mengine, iliongeza matumizi katika sekta ya afya na huduma za jamii. Deni la Serikali limeongezeka na kufikia shilingi bilioni 817.5 mwezi Aprili 2020, kutoka shilingi bilioni 806.6 mwishoni mwa Juni 2019, kutokana zaidi na mikopo mipya.

Urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 21.1 katika





kipindi cha Julai 2019 hadi Aprili 2020, ikiwa ni pungufu ya nakisi ya dola za Marekani milioni 38.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2018/19. Hali hii ilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa mapato ya mauzo ya karafuu na huduma nje ya nchi. Mapato ya mauzo ya nje ya nchi yalikua kwa asilimia 31.8 hadi dola za Marekani milioni 213.1. Aidha, uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi uliongezeka kwa asilimia 32.6 na kufikia dola za Marekani milioni 329.0, hali iliyochangiwa na kuongezeka kwa uagizaji wa ngano, mchele, sukari na mashine.

### **Utekelezaji wa Malengo ya Sera ya Fedha ya Mwaka 2019/20**

Katika mwaka 2019/20, Benki kuu iliendelea kutekeleza sera ya fedha yenye lengo la kuhakikisha mfumuko wa bei unabakia kuwa tulivu ndani ya lengo la muda wa kati la asilimia 5.0, ambao ni mchango muhimu katika kusaidia ukuaji endelevu wa uchumi wa asilimia 7.0. Ili kutimiza haya, Benki Kuu ililenga kutekeleza sera ya fedha yenye malengo yafuatayo:

- i. ukuaji wa fedha taslim wa asilimia 9.0;
- ii. ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) wa asilimia 10.0;
- iii. ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia 13.5; na
- iv. kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne.



Utekelezaji wa sera ya fedha kwa kipindi cha mwaka 2019/20 ulikuwa sambamba na malengo, licha ya changamoto zilizosababishwa na janga la ugonjwa wa COVID-19. Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Aprili 2020, Benki Kuu iliendelea kutekeleza sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi kwenye uchumi kwa ajili ya kuwezesha benki na taasisi za fedha kuongeza utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi na kukuza shughuli mbalimbali za kiuchumi. Aidha, Benki Kuu iliongeza zaidi utoaji wa ukwasi katika nusu ya pili ya mwaka 2019/20, ili kuunusuru uchumi na athari za mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19. Hatua kadhaa zilizochukuliwa ndani ya mwaka 2019/20 ni pamoja na kushusha kiwango cha chini cha kisheria cha sehemu ya amana kinachotakiwa kuwekwa Benki Kuu kutoka asilimia 8.0 hadi 6.0 na kupunguza kiwango cha riba kinachotozwa kwa benki kukopa Benki Kuu (*discount rate*) kutoka asilimia 7.0 hadi asilimia 5.0. Vilevile, Benki Kuu iliongeza unafuu kwenye dhamana na hati fungani za serikali zinazotumika na benki kama dhamana wakati wa kukopa kutoka Benki Kuu, kwa kupunguza kiwango cha dhamana kutoka asilimia 10.0 hadi asilimia 5.0 kwa dhamana zinazoiva ndani ya mwaka mmoja na kutoka asilimia 40.0 hadi asilimia 20.0 kwa dhamana zinazoiva baada ya mwaka mmoja. Aidha, Benki Kuu iliongeza matumizi ya nyenzo za sera ya fedha katika kuongeza ukwasi ikiwamo kuendelea kutoa mikopo ya muda mfupi kwa mabenki. Mbali na hatua za kuongeza ukwasi zilizolenga kuboresha mizania za sekta ya benki na utoaji wa mikopo kwa riba nafuu, benki pia zilipewa unafuu wa kikanuni katika kufanya marekebisho ya marejesho ya mikopo.



Hatua hizi za sera ya fedha zimesaidia kuboresha hali ya ukwasi kwenye uchumi pamoja na kusaidia kupungua kwa wa riba katika masoko ya fedha. Riba ya siku moja katika soko la fedha baina ya mabanki (*overnight interbank cash market rate*) kwa mwezi Aprili 2020 ilikuwa asilimia 4.83 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.47 mwezi Juni 2019 na asilimia 5.20 mwezi Aprili 2019. Vilevile, wastani wa riba za dhamana za serikali zilipungua na kufikia asilimia 4.88 mwezi Aprili 2020, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 8.69 mwezi Juni 2019 na asilimia 8.20 mwezi Aprili 2019. Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Aprili 2020, wastani wa riba za mikopo inayotolewa na mabanki imeendelea kupungua japo kwa kasi ndogo na kufikia asilimia 16.85 ikilinganishwa na asilimia 17.16 katika kipindi kama hicho mwaka 2018/19.

Sambamba na utekelezaji wa sera ya fedha iliyolenga kuongeza ukwasi, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi, M3, uliongezeka kwa wastani wa asilimia 9.9 katika kipindi cha Julai 2019 hadi Aprili 2020, ikilinganishwa na lengo la asilimia 10.0 kwa mwaka unaoishia Juni 2020. Aidha, ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulikuwa wa wastani wa asilimia 8.7, dhidi ya lengo la asilimia 13.5.

Thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu mbalimbali duniani imeendelea kuwa tulivu katika kipindi chote cha kuanzia mwezi Julai 2019 hadi Aprili 2020, ikibadilishwa kati ya shilingi 2,299.3 na shilingi 2,302.7 kwa dola moja ya Marekani ikilinganishwa na shilingi 2,276.4 hadi Shilingi 2,300.9 kwa dola moja ya Marekani katika kipindi kama hicho mwaka 2018/19. Utulivu huu wa shilingi ulitokana na utekelezaji wa sera madhubuti ya fedha, usimamizi



kwenye kuhakikisha uwazi na utaratibu mzuri katika soko la kubadilisha fedha za kigeni, kuimarika kwa urari wa biashara pamoja na kupungua kwa bei ya mafuta katika soko la dunia.

### ***Matarajio ya Uchumi na Malengo ya Sera ya Fedha ya Mwaka 2020/21***

Makadirio ya viashiria vya uchumi mpana kwa mwaka 2020/21 umezingatia athari za janga la ugonjwa wa COVID-19 katika uchumi wa dunia na athari zake kwa uchumi wa Tanzania. Vilevile, makadirio haya yamezingatia mazingira ya uchumi wa nchi na utekezaji wa sera na mikakati inayowiana na mipango ya maendeleo ya Serikali.

Katika mwaka 2020/21, Serikali inalenga kufikia malengo ya kiuchumi yafuatayo:

- i. ukuaji wa Pato halisi la Taifa la asilimia 5.5 kwa Tanzania bara kwa mwaka 2020;
- ii. mfumuko wa bei ulio ndani ya kiwango cha tarakimu moja, kati ya wastani wa asilimia 3.0 hadi 5.0; na
- iii. nakisi ya bajeti, ikijumuisha misaada kutoka nje (*grants*), ya asilimia 2.6 ya Pato la Taifa kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa mwaka 2020/21.

Kwa upande wa uchumi wa Zanzibar, Serikali inalenga kufikia malengo yafuatayo:

- i. ukuaji wa Pato la Taifa wa asilimia 5.0 mwaka 2020;
- ii. mfumuko wa bei ulio ndani ya kiwango cha tarakimu moja; na



- iii. nakisi ya bajeti ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, ikijumuisha misaada kutoka nje (*grants*), ya kati ya asilimia 3.0 hadi 5.0 ya Pato la Taifa mwaka 2020/21.

Kwa kuzingatia mazingira ya kupungua kwa bei za mafuta katika soko la dunia, na matarajio ya mfumuko wa bei kuendelea kuwa tulivu na kubaki katika viwango vya tarakimu moja, Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kutekeleza sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi ili kuchochea na kuimarisha shughuli mbalimbali za kiuchumi. Ili kufikia malengo haya kwa mwaka 2020/21, Benki Kuu imepanga kufikia malengo yafuatayo:

- i. ukuaji wa fedha taslim wa asilimia 9.5;
- ii. ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) wa asilimia 10.0;
- iii. ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia 11.6; na
- iv. kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Katika utekelezaji wa majukumu yake, Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kuboresha ufanisi wa masoko ya fedha ikiwa ni pamoja na miundombinu yake na kutoa elimu kwa umma. Vilevile, Benki Kuu itaendelea kutekeleza sera ya fedha kwa uwazi na kwa kutumia nyenzo mbalimbali za sera ya fedha ili kuhakikisha kuwa uchumi unakuwa na ukwasi wa kutosha kulingana na mahitaji mbalimbali ya wakati huo, na kudumisha utulivu wa riba katika soko la fedha.



## Hitimisho

Uchumi wa Tanzania umeendelea kuwa imara katika mwaka 2019, kama ilivyokuwa kwa miaka ya hivi karibuni. Aidha, katika nusu ya kwanza ya mwaka 2020 uchumi umekumbwa na changamoto zilizotokana na athari za ugonjwa wa COVID-19, japo athari hizi hazikuwa kubwa sana kutokana na maamuzi ya Serikali ya kutofunga shughuli za uzalishaji (*lockdown*), pamoja na uchumi kutegemea sekta mbalimbali (*diversified economy*). Kutokana na sababu hizi, pamoja na kuanza kufunguliwa kwa shughuli za kiuchumi kwa washirika wa kibiashara katika nusu ya pili ya 2020, ukuaji wa uchumi unakadiriwa kuendelea kuwa imara katika mwaka 2020 japo ukiongezeka kwa kasi ndogo ikilinganishwa na mwaka 2019. Uchumi unakadiriwa kukua kwa asilimia 5.5 mwaka 2020, ikilinganishwa na makadirio ya awali ya asilimia 6.9 kabla ya mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19.

Mfumuko wa bei unakadiriwa kubakia ndani ya lengo la muda wa kati la asilimia 5.0 kwa mwaka 2020/21, ikichangiwa zaidi na wastani wa bei ndogo ya mafuta katika soko la dunia, upatikanaji wa chakula cha kutosha, utulivu wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya fedha za kigeni, na kufunguka kwa uchumi wa dunia baada ya shughuli nyingi kufungwa kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19. Aidha, Benki Kuu itaendelea kutekeleza sera ya fedha yenye lengo la kuongeza ukwasi kwenye uchumi ili kusaidia shughuli za uchumi, pamoja na kudumisha utulivu wa sekta ya fedha. Benki Kuu itaendelea kufuatilia kwa karibu athari za mlipuko



wa COVID-19 kwenye sekta mbalimbali za uchumi na kuchukua hatua stahiki ili kupunguza athari kwenye uchumi. Kwa kuzingatia mwenendo wa uchumi, pamoja na utekelezaji thabiti wa sera ya fedha na kibajeti, Benki Kuu ina matumaini kwamba malengo ya sera ya fedha yaliyowekwa katika Tamko hili la mwaka 2020/21 yatafikiwa.











Kwa maelezo zaidi wasiliana na:  
Mkurugenzi wa Utafiti na Sera za Uchumi  
Benki Kuu ya Tanzania, 2 Mtaa wa Mirambo, 11884 Dar es Salaam  
Simu: +255 22 2233328, +255 22 2233350, Nukushi: +255 22 2234060  
Tovuti: <http://www.bot.go.tz>